Jina ........................................................................................................ Nambari ................................................

Shule ........................................................................................................ Sahihi ................................................

Tarehe ................................................

102/3

**KISWAHILI**
KARATASI YA TATU
**Julai / Agosti 2016**
Muda: Saa 2½

# TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA KERICHO MAGHARIBI

## Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

**Kidato cha Nne**

**KISWAHILI**

Karatasi - 102/3

**Julai / Agosti 2016**

**Muda :** Saa 2½

## MAAGIZO

1. Jibu maswali MANNE pekee.
2. Swali la KWANZA ni la LAZIMA.
3. Kisha chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizobakia; yaani Riwaya, Hadithi Fupi, Tamthilia na Fasihi Simulizi.
4. Usijibu maswali MAWILI kutoka SEHEMU MOJA.
5. Kila swali lina alama 20
6. Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
7. Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.
8. Watahiniwa wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**MTAHINI PEKEE.**

| | SEHEMU | UPEO | ALAMA | MTAHINI |
|---|---|---|---|---|
| A | USHAIRI | 20 | | |
| B | RIWAYA | 20 | | |
| C | HADITHI FUPI | 20 | | |
| D | TAHMTHILIA | 20 | | |
| E | FASIHI SIMULIZI | 20 | | |
| | JUMLA | 80 | | |

1. **LAZIMA : SEHEMU YA 'A'**
**USHAIRI**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Kila mikaapo hushika tama
Na kuiwazia hali inayonizunguka
Huyawazia madhila
Huziwazia shida.
Huiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi
Shida ya kudhalilishwa kazini
Madhila ya kufanyiwa dharau
Kwa sababu ya jinsia ya kike

Hukaa na kujidadisi
Hujidadisi kujua kwa nini
Jamii haikisikii kilio changu
Wenzangu hawanishiki mikono
Bali wananidharau kwa kuukosoa utamaduni

Hukaa na kujiuliza
I wapi afua yangu dunia hii
I wapi raha yangu ulimwengu huu
I wapi jamaa nzima ya wanawake?

**MASWALI**

i) Pendekeza kichwa kwa shairi hili. (alama 2)

ii) Shairi hii ni la aina gani? Eleza. (alama 3)

iii) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)

iv) Taja mishata yoyote miwili iliyotumika katika shairi hili. (alama 2)

v) Toa mifano ya mbinu za kifasihi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)

vi) Tambua nafasi-neni katika shairi hili. (alama 2)

vii) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

**SEHEMU YA B**
**RIWAYA:**
**<u>Kidagaa kimemwozea ;</u> *Ken Walibora***
**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** "Afrika huru ina watu wachache wenye nguvu na uwezo mwingi juu ya wengi. Wachache hawa hawaogopi, ashakum si matusi, hata kutema mate au kumwaga mkojo usoni mwa haki, usawa na uhuru uliopiganiwa na kumwagiwa damu . . . "

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Ukirejelea riwaya '*Kidagaa kimemwozea,*' dhihirisha namna ambavyo haki za wengi zimekiukwa. (alama 16)

**3.** Udhalimu ni maudhui makuu katika riwaya ya '*Kidagaa kimemwozea,*' (alama 20)

**SEHEMU YA C**
**HADITHI FUPI**
**<u>Damu Nyeusi na Hadithi nyingine</u> ; *Ken Walibora na Said A. Mohamed***

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** 'Asasi ya ndoa imekumbwa na vizingiti mbalimbali katika jamii ya kisasa.' Tetea kaulli hii ukirejelea hadithi zifuatazo. (alama 20)

a) Mwana wa Darubini

b) Mke wangu

c) Maeko

d) Masikini Babu yangu

**5.** "Aaa, ikiwezekana, isiwezekane, yeye ataomba zawadi kubwa ingawa pengine ni ndogo kwa mzee yule. Zawadi ya kuchukuliwa Uingereza.

a) Eleza muktadha na dondoo hili. (alama 4)

b) Dhihirisha namna ambavyo ndoto ya kuchukuliwa Uingereza ulivyogeuka karaha kwa mrejelewa. (alama 16)

**SEHEMU YA D:**
**TAMTHILIA:**
**Mstahiki Meya** ***: Timothy M. Arege***
**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** "Si habari za kwenda nyumbani" Nimeona niache hii kazi . . . "

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili: (alama 4)

b) Bainisha sababu anazotoa mnenaji za kuacha kazi. (alama 10)

c) Eleza sifa na umuhimu wa mnenewa. (alama 6)

**7.** 'Msiba wa kujitakia hauna kilio' Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea tamthilia ya *Mstahiki Meya.* (alama 20)

**SEHEMU YA E:**
**FASIHI SIMULIZI**

**8.** a) Eleza umuhimu wa kufanya utafiti wa Fasih Simulizi nyanjani. (alama 7)

b) Eleza maandalizi mabayo mtafiti anafaa kufanya kabla ya kwenda nyanjani. (alama 7)

c) Dhihirisha baadhi ya vikwazo ambavyo mtafiti anaweza kukabiliania navyo wakati anapofanya utafiti. (alama 20)